JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

# MKUTANO WA SITA WA JUKWAA LA TAIFA LA WADAU WA SEKTA MTAMBUKA KATIKA USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI



## MUHTASARI

Kaulimbiu: “Mafuriko na Ukame: Uwekezaji katika Usalama wa Maji ni Suala la Haraka”





11-12 Februari 2024

Mahali: Ukumbi Mpya wa Maktaba-Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam

Washirika wa kimkakati

Global Water Partnership Southern Africa
Tanzania Water Partnership

water for people

SHAHIDI WA MAJI

# UTANGULIZI

Mkutano wa sita (6) wa Jukwaa la Taifa la Wadau wa Sekta Mtambuka katika Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji *(National Multi-Sectoral Forum (NMSF) on Water Resources Management and Development)* ulifanyika tarehe 11 na 12 Februari 2024, katika ukumbi wa Maktaba mpya ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam, Tanzania.

Lengo la Jukwaa hili ni kuleta pamoja sekta zote zinazohusiana na maji na wadau ili kwa pamoja waweze kujadili changamoto mbalimbali; kubadilishana maarifa na uzoefu; kuboresha uratibu; na kuongeza ushirikiano katika maeneo mbalimbali yanayohusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2017, Jukwaa hilo limetumika kama nyenzo muhimu ya kushughulikia changamoto mbalimbali zinazokabili usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

Mgeni rasmi katika Mkutano huo alikuwa Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kaulimbiu ya mkutano huo ilikuwa "*Mafuriko na Ukame: Uwekezaji katika Usalama wa Maji ni Suala la Haraka.*"

Kaulimbiu hiyo ililenga kuweka mikakati ya haraka katika kukabiliana na ongezeko la maafa yanayotokana na mafuriko yanayojitokeza mara kwa mara nchini Tanzania na kulipa kipaumbele suala la uhakika wa maji kupitia uwekezaji.

Malengo mahususi ya Mkutano wa Jukwaa wa mwaka 2024 yalikuwa ni pamoja na; kubainisha mikakati madhubuti ya usimamizi wa mafuriko na ukame; kujadiliana juu ya kuweka suala la usalama wa maji katika ajenda ya usalama wa taifa; kuchochea ushiriki wa sekta binafsi katika kuhakikisha usalama wa maji; kupitia utekelezaji wa Tamko la Mbeya la Mawaziri wa Sekta zinazohusiana na maji; na kuthibitisha mikakati ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za sekta ndogo ya rasilimali za maji iliyoandaliwa na Vikundi Kazi vya Jukwaa.

Mkutano ulifanyika kwa muda wa siku mbili (2) na ulikuwa umegawanyika katika mada kuu saba (7) ambapo mawasilisho ya mada katika nyanja mbalimbali yalifanyika na kufuatiwa na mijadala ya wadau.

# Mada ya 1: Ufunguzi

- Jukwaa la Taifa la Sekta Mtambuka (NMSF) ni jukwaa muhimu linalohusisha sekta na wadau mbalimbali katika kuweka mikakati na mipango fanisi na endelevu ya usimamizi na uendelezaji wa pamoja wa rasilimali za maji nchini.
- Maji, Nishati na Chakula vinahusiana moja kwa moja na kutegemeana kwa karibu, hivyo uwepo wa mipango na uwekezaji jumuishi wa sekta hizi_ (*Water, Energy, and Food Nexus*) ni muhimu ili kuhakikisha uwekezaji wenye tija na endelevu katika usalama wa maji.
- Ushiriki wa wadau katika Jukwaa unahitaji kuongezwa ili kujumuisha washiriki zaidi kutoka sekta binafsi za ndani na washirika wa maendeleo wa kitaifa na kimataifa.
- Kuna umuhimu wa kuandaa haraka Mpango wa Taifa Himilivu wa Maji (*National Water Resilience Program*), utakaozingatia majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.
- Asilimia 57 ya Pato la Taifa huathiriwa na mabadiliko ya tabianchi hasa kutokana na majanga yanayohusiana na maji.
- Miundombinu ya kuhifadhi maji kama vile mabwawa inaweza kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi hivyo kuna haja ya kuwekeza katika ujenzi wa mabwawa mengine makubwa 10 ya kimkakati yenye uwezo wa kulinganishwa na Bwawa la Julius Nyerere au Bwawa la Mtera.
- Rasimu ya Mpango wa Uwekezaji katika Maji Tanzania inalenga kufikia uhakika wa maji kitaifa na kustahimili mabadiliko ya tabia nchi kupitia uwekezaji ulioratibiwa wenye bajeti ya jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 15 katika sekta zinazohusiana na maji.

- Ni muhimu kupitia na kufanya tathmini upya ya mamlaka na mgawanyo wa majukumu ya kisekta ili kuongeza uwajibikaji, kuimarisha uwezo na mbinu za kutafuta fedha kutoka vyanzo vipya, na kujumuisha matumizi ya maarifa ya asili (*indigenous knowledge*) na ushiriki wa jamii katika kuandaa mikakati mbalimbali.
- Serikali imedhamiria kuwekeza katika mikakati endelevu ya usimamizi wa rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na kupitia na kuboresha mipango ya kisekta iwe jumuishi na kuhimiza uwekezaji katika teknolojia za uvunaji wa maji ya mvua.
- Maazimio ya Mkutano wa 6 wa Jukwaa ikijumuisha ajenda ya uhakika wa maji yawasilishwe Ofisi ya Waziri Mkuu na katika Kikao cha Baraza la Mawaziri.

# Mada ya 2: Kudhibiti Mafuriko na Ukame katika Mabadiliko ya Tabianchi

- Kuna umuhimu wa haraka wa kuwekeza katika teknolojia za utabiri sahihi wa majanga.
- Ukusanyaji na ufuatiliaji wa takwimu za hali ya hewa na maji unapaswa kuimarishwa ili kuboresha utayari wa kukabiliana na majanga yanayohusiana na maji.
- Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa sekta ya maji ili kutumia vyema taarifa zinazotokana na satelaiti pamoja na mifumo ya kuangalia mafuriko na ukame inayotokana na satelaiti ili kuziba pengo la upungufu wa taarifa.
- Ni muhimu kuimarisha mifumo ya kisheria, kuweka kipaumbele katika utafiti, elimu, na mafunzo, kukuza ushirikiano baina ya sekta mbalimbali, na kuhakikisha ushirikiano kutoka kwa washirika wa kimataifa ili kuboresha ufanisi wa mifumo ya tahadhari za mapema kwa majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi.
- Kusimamia utekelezaji wa sheria na viwango katika ujenzi na mipango miji; kuongeza ushiriki wa jamii katika uhifadhi wa mazingira; kuboresha mifumo ya mifereji na miundombinu ya maji ili kuzuia upotevu wa maji; kutumia mbinu za kilimo zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi; na kusimamia rasilimali za maji kwa ufanisi ili kupunguza hatari za mafuriko na ukame.
- Kipaumbele kiongezwe katika utafiti tumizi (applied research) unaotoa majibu kwa matatizo yaliyopo kuliko utafiti wa kawaida (basic research) ili kukabiliana na changamoto katika sekta ya maji na mazingira, na kuwezesha matumizi ya bunifu (innovations) mbalimbali zinazoibuliwa katika sekta ya maji.

# Mada ya 3: Mabadiliko ya Matumizi ya Ardhi na Athari zake katika Mafuriko na Ukame.

- Kuboresha matumizi ya ardhi kwa kutumia mbinu endelevu kama vile uhifadhi wa maeneo ya mito na vyanzo vya maji, urejeshaji wa ardhi iliyoharibika kwa kupanda miti asilia rafiki wa maji na kutumia mbinu za kilimo hifadhi, kuweka miundombinu ya kuvuna na kuhifadhi wa maji ya mvua katika mipango ya maendeleo, na kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya uoto wa asili na matumizi ya ardhi.
- Kuweka na kutekeleza sera za uhifadhi wa mazingira zinazozingatia taarifa sahihi, hasa katika uhifadhi na ulinzi wa maeneo ya mito.
- Kuweka na kutekeleza skimu za kutoa motisha kwa wadau na wakulima wanaotumia mbinu bora na matumizi fanisi ya maji.
- Kujenga ujuzi na maarifa kwa wakulima wadogo kuhusu matumizi fanisi ya maji na mbinu endelevu za kilimo.
- Kujenga uelewa na ufahamu miongoni mwa wadau kuhusu maana na umuhimu wa vyanzo vya maji.
- Kuimarisha ushiriki wa wadau katika kuandaa kanuni mbalimbali za utekelezji kupitia mchakato wa wazi na unaoruhusu mabadiliko ya mara kwa mara inapobidi.

# MAAGIZO YA WAZIRI MKUU KATIKA MKUTANO WA SITA (6) WA JUKWAA LA TAIFA LA SEKTA MTAMBUKA KATIKA USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI

1. Wizara ya Maji iongeze kasi katika uwekezaji wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua na kuandaa taarifa ya Mkutano wa 6 wa Jukwaa na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya majadiliano katika Baraza la Mawaziri.

2. Bodi za Maji za Mabonde ziimarishe juhudi za uhifadhi wa rasilimali za maji kwa kuweka mipaka na kulinda vyanzo vya maji kisheria kwa kutangaza katika Gazeti la Serikali, na kwa kupanda miti rafiki kwa maji katika maeneo yote ya vyanzo vya maji.

3. Wizara ya Maji ishirikiane na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Idara ya Usimamizi wa Maafa katika kuimarisha uwekezaji wa mifumo ya kudhibiti na kutabiri maafa yanayotokana na maji.

4. Wizara ya Maji iongeze uelewa kwa umma/wananchi kuhusu usimamizi shirirkishi, endelevu na himilivu wa rasilimali za maji.

5. Mamlaka za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira kushughulikia tatizo la upotevu wa maji (non revenue water).

6. Halmashauri za Wilaya, Jiji, na Manispaa zishirikiane na Wizara ya Maji katika kulinda vyanzo vya maji dhidi ya uvamizi na uchafuzi wa mazingira.

7. Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iache kutoa vibali vya matumizi ya ardhi na ujenzi katika maeneo ya vyanzo vya maji na maeneo ya kingo za mito. Wizara hiyo itashirikiana na Wizara ya Maji kuhakikisha shughuli hizo zinasitishwa mara moja.

8. Wizara ya Maliasili na Utalii iache kutoa vibali vya uvunaji wa misitu katika maeneo ya vyanzo vya maji, kudhibiti kilimo cha miti biashara katika vyanzo vya maji, na kuhakikisha uzalishaji miche na upandaji wa miti rafiki kwa maji katika maeneo ya vyanzo vya maji.







# MAAGIZO YA WAZIRI MKUU KATIKA MKUTANO WA 6 WA JUKWAA LA TAIFA LA SEKTA MTAMBUKA







9. Wizara ya Mifugo kuimarisha ufugaji wenye tija na endelevu kwa kuzingatia uwezo wa ardhi iliyopo, kujenga miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo, na kuzuia unyweshaji wa mifugo katika vyanzo vya maji moja kwa moja.

10. Wizara ya Kilimo kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji kwa ajili ya umwagiliaji, na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji ili kuzuzia upotevu wa maji na kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji.

11. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na Wizara ya Kilimo kutoa viwango vya mahitaji ya maji kwa mazao yanayolimwa kwa wingi (crop water requirement), kuhimiza matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi wa maji, na kuelimisha jamii kuhusu kilimo endelevu na mbinu za umwagiliaji zinazopunguza mmomonyoko wa udongo.

12. Wizara ya Madini kusitisha shughuli za uchimbaji haramu wa madini, hasa katika maeneo ya vyanzo vya maji, hususan kwa wachimbaji wadogo.

13. Wamiliki wa mabwawa wasajili mabwawa yao kwa mamlaka husika na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa ajili ya usalama wa mabwawa hayo.

14. Sekta zote kuongeza ushirikiano wa kisekta katika miradi yao inayohusiana na maji, kuandaa mipango ya pamoja, na kutekeleza Mipango ya Usimamizi na Maendeleo ya Rasilimali za Maji (IWRM) na Mipango ya Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji (2021-2035) katika mabonde yote tisa. Kila sekta lazima itenge fedha za bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa mipango hiyo na kutoa taarifa za maendeleo katika Mikutano ya Mwaka ya Jukwaa.

15. Mipango ya kisekta iliyopo ya uwekezaji kupitiwa upya, kuanishwa kuwa jumuishi na kuratibiwa vyema

# Mada ya 4: Tafakuri na Hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji wa shughuli za Jukwaa na Tamko la Mbeya la Mawaziri wa Kisekta

- Programu ya Global Water Leadership (GWL) iliyoongozwa na GWPTZ ilijikita katika kuimarisha ushirikiano baina ya sekta kupitia Jukwaa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na maendeleo endelevu.
- GWL ilisaidia vikundi kazi vya Jukwaa kutambua vikwazo vikuu vitatu katika usimamizi na uendelezaji endelevu wa rasilimali za maji unaostahimili mabadiliko ya tabianchi. Vikwazo hivyo ni (1) ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, (2) mbinu na matumizi ya miundombinu isiyofaa ya kilimo na umwagiliaji - Bonde la Wami/Ruvu, na (3) muingiliano wa majukumu ya kisheria, kiutendaji na kiudhibiti yanayoathiri ushirikiano baina ya sekta.
- Vikundi kazi vya Jukwaa vilitengeneza mikakati ya kina ya kukabiliana na vikwazo hivyo, ikijumuisha mipango ya utekelezaji na kifedha.
- Sababu za msingi za ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji ni pamoja na usawa katika mgao wa rasilimali fedha, kutotambua thamani ya kiuchumi ya maji, uwezo hafifu wa kiufundi wa kuandaa maandiko yanayoweza kupata fedha, uratibu mdogo kati ya sekta zinazotumia maji, na athari za mabadiliko ya tabianchi.
- Hatua za kushughulikia vikwazo hivyo ni pamoja na kujenga uwezo wa kutafuta rasilimali fedha, kubainisha thamani ya kiuchumi ya maji na kuandaa mipango na utekelezaji wa programu za usalama wa maji kwa gharama ya jumla ya TZS bilioni 72.
- Sababu za msingi za matumizi na mbinu zisizofaa za umwagiliaji kwa kesi ya Bonde dogo la Ruvu ni pamoja na miundombinu ya umwagiliaji iliyopitwa na wakati, ukosefu wa utaalamu wa kiufundi miongoni mwa vikundi vya watumiaji wa maji, na ufahamu mdogo wa mbinu za kisasa za matumizi fanisi ya maji kwenye kilimo.
- Hatua zilizopendekezwa ni pamoja na kuanzisha mifumo ya umwagiliaji ya kisasa, yenye ufanisi, na ya gharama nafuu, pamoja na kuimarisha uwezo wa kiufundi wa vikundi vya watumiaji wa maji, kwa bajeti ya TZS bilioni 463.
- Sababu za msingi za kuingiliana kwa mamlaka kisheria ni pamoja na utekelezaji usio na mpangilio wa mifumo, kuingiliana kwa majukumu ya kisekta, na uwepo wa rasilimali chache. Hatua zilizopendekezwa ni pamoja na kupitia upya mifumo ya kisheria na kitaasisi, kuimarisha uratibu wa kisekta, kutumia vyema rasilimali zilizopo kwa bajeti ya takriban TZS bilioni 2.

# Mada ya 5: Uhakika wa Maji Tanzania na Mpango Shirikishi wa Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji wa Bonde la Ziwa Victoria

- Uwekezaji jumuishi unahitajika katika miradi ya kimkakati ya ujenzi wa mabwawa ikiwa ni pamoja na mabwawa ya Farkwa, Songwe Chini, Kidunda, na Farkwa ambapo usanifu wa kina umeshafanyika, pamoja na Mipango ya Usafirishaji wa Maji baina ya Mabonde (Inter Basin Water Transfer) ikiwa ni kuyatoa kwenye mabonde yenye maji mengi na kuyaleta kwenye mabonde yenye maji kidogo ili kuimarisha usalama wa maji.
- Kuimarisha mitandao ya ufuatiliaji wa maji na kuendeleza mifumo ya ushirikiano na kubadilishana taarifa na nchi jirani.

# Mada ya 6: Uhikaka wa Maji kuwa suala la Usalama wa Taifa

- Maji yanaunganisha nyanja zote za maisha ya mwanadamu, ikiwemo afya, kilimo, nishati, chakula, maendeleo ya kiuchumi, na amani.
- Maji yanaweza kusababisha migogoro ya kitaifa na kimataifa, hivyo uhikika wa maji ni suala la amani na usalama wa taifa.
- Mradi wa Uhikika wa Maji Dar Es Salaam (DarWRP) utatumika kama mfano wa kuimarisha usalama wa maji katika bonde la Wami/Ruvu kupitia ushiriki wa sekta mtambuka ikiwemo sekta binafsi.
- Kuendeleza mikakati ya muda mrefu ya uhakika wa maji ambayo inadumu zaidi ya masuala ya kisiasa ya muda mfupi.
- Kuunganisha mikakati ya usimamizi wa rasilimali za maji katika mipango ya maendeleo ya vijiji na kata ili kuhakikisha usalama wa maji.
- Kuongeza ushirikiano na taasisi za kitaaluma na kiutafiti ili kusaidia mipango ya uhakika wa maji kwa kutumia mikakati inayozingatia taarifa sahihi.
- Kuanzisha ajenda ya kitaifa ya usalama wa maji ili kuweka kipaumbele masuala ya maji katika mijadala ya kitaifa.
- Kutambua maji kama rasilimali adhimu na muhimu ya kitaifa na kuiingiza katika Hazina ya Taifa.
- Kuweka mizania katika usimamizi wa rasilimali za maji na uwekezaji katika miradi ya usambazaji maji kwa ajili ya uhakika wa maji wa muda mrefu.
- Kuandaa na kutekeleza viashiria vya wazi vya utendaji kazi vya usalama wa maji katika ngazi zote za usimamizi wa rasilimali za maji na katika serikali za mitaa ili kuimarisha ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha uwajibikaji.
- Kuimarisha uwazi katika kufanya maamuzi na kutenga rasilimali fedha, ili kurahisisha utekelezaji wa miradi na kupunguza ukiritimba na urasimu.
- Kukuza utamaduni wa ushirikiano wa kisekta ili kuratibu juhudi, rasilimali watu na fedha, kuepuka urudufu, na kuleta matokeo chanya katika malengo ya uhakika wa maji wa kitaifa.
- Kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ambayo hutenganisha maeneo kwa ajili ya mabwawa, makazi, na kilimo, hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira na hatari za mafuriko.

# Mada ya 7: Maazimio ya Mkutano wa 6 wa Jukwaa na Kufunga

- Utekelezaji wa mapendekezo jukwaa na maagizo ya Mgeni Rasmi - Waziri Mkuu na utekelezaji wa Mkakati wa kukabiliana na changamoto ulioandaliwa na Vikundi Kazi vya Jukwaa.
- Wadau wote wa sekta mbalimbali ikiwemo wizara zinazohusiana na maji kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji maelekezo na mikakati ya Jukwaa na kusaidia shughuli zake, ikiwemo zile za vikundi kazi.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI

WASILIANA NASI:www.maji.go.tz/ ps@maji.go.tz
| Mji wa Serikali | Mtaa wa Maji | SLP 456 Dodoma

majiDigital Tanzania    Wizarayamajitz    @maji_mowi